**HOTUBA YA MKUU WA WILAYA WA MPWAPWA MH. JABIR M. SHEKIMWERI YA UFUNGUZI WA KIKAO KAZI KUHUSU MAFUNZO YA AWALI YA UJUMUISHWAJI WA AFUA ZA LISHE KATIKA MIPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

**Ndugu,**
*Mwenyekiti wa Halmashauri,*
*Katibu Tawala wa Wilaya,*
*Mkurugenzi wa Halmashauri Wilaya,*
*Mganga mkuu wa Wilaya,*
*Wawezeshaji wa Kitaifa*

*Wajumbe wa Kamati za Lishe kutoka ngazi ya Halmashauri*

*Wadau wetu wa Maendeleo – ACTION AGAINST HUNGER.*

*Mabibi na Mabwana*

Awali ya yote napenda nichukue fursa hii kuwashukuru kwa kunialika katika kikao hiki cha maandalizi ya awali ya ujumishwaji wa afua za lishe katika mipango na bajeti ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/20. Napenda pia kuishukuru Serikali kupitia shirika la ACTION AGAINST HUNGER kwa kuona umuhimu wa kuwezesha mafunzo haya; hii ni hatua muhimu sana katika uboreshaji wa shughuli za lishe Wilayani hapa. Aidha, kwa wale wanaotoka nje ya Halmashauri yetu nawapeni pole kwa safari na nasema karibuni sana

*Ndugu washiriki,*
Sote tunaelewa wazi kuwa pamoja na maendeleo ambayo nchi yetu imekuwa ikiyapata katika maeneo mbalimbali, bado utapiamlo umeendelea kuathiri jamii ya ki-Tanzania hususan kiafya, kielimu na kiuchumi; hivyo kukwamisha kasi ya kupungua kwa umaskini nchini kuwa si ya kuridhisha.

*Ndugu washiriki,*

Lishe ni mchakato unahusisha jinsi mwili unavyokitumia chakula kilicholiwa. Hatua hizi ni tangu chakula kinapoliwa, jinsi mwili unavyokisaga na kuyeyusha na hatimaye virutubishi kufyonzwa na kutumika mwilini.

Utapiamlo ni hali ya Lishe duni inayotokana na kuzidi au kupungua kwa virutubishi mwilini.

Lishe duni si tu inaathiri maendeleo ya mtoto lakini pia inaathiri ukuaji wake kimwili na kiakili toka kipindi cha ujauzito na hatimaye kuathiri mchango wake katika maendeleo ya taifa kwa kipindi chote cha uhai wake.

*Ndugu washiriki,*

Takwimu za 30/06/2018 katika zoezi la Upimaji wa Hali ya Lishe, utoaji wa dawa za minyoo na matone ya Vitamin A zimebaini kuwa utapiamlo bado ni tatizo kubwa linaloathiri watoto walio na umri chini ya miaka mitano hapa Wilayani Mpwapwa. Kwa mujibu wa takwimu; Udumavu ni asilimia **37**, Uzito pungufu ni asilimia **12**, Wakondefu ni asilimia **1**.

Hali hii ni mbaya na inahitaji nguvu kubwa ielekezwe kupunguza tatizo la utapiamlo kwa watoto wetu ambao ndo nguvu kazi ya taifa la kesho.

*Ndugu washiriki,*

Hali ya lishe ya wanawake walio katika umri wa uzazi (miaka 15-49) nayo bado ni mbaya; sote tunajua, hali ya lishe ya mama ikiwa mbaya inaadhiri hali ya mtoto toka tumboni pamoja na malezi na makuzi ya mtoto. Tafiti za hivi karibuni zimebaini kwamba,kati ya wanawake kumi, wastani wa wawili wana utapiamlo.

Lishe duni kwa wanawake wajawazito inachochea hatari ya kujifungua watoto njiti, waliodumaa au kuharibu mimba. Asilimia 30 ya wanawake walio katika umri wa kuzaa wana upungufu wa damu unaochangia kupoteza maisha wakati au baada ya kujifungua. Vifo vya wanawake

wajawazito vitapungua sana endapo watakuwa na hali nzuri ya lishe katika kipindi chote cha ujauzito na baada ya kujifungua.
Pia ni asilimia chini 30 ndo wanatumia chumvi yenye madini joto ya kutosha, aidha asilimia hizo za uchunguzi wa kimaabara zina dhihirisha kuwa bado hali hairidhishi kwa upande wa matumizi ya chumvi yenye madini joto katika kaya. Tatizo hili lisipodhibitiwa mapema linaweza likaathiri uwezo wa watoto wetu katika kutenda na kufundishika hasa wanapofikia umri wa kwenda shule. Kupitia kikao hiki ninaagiza mipango yenu ilenge pia kudhibiti uuzwaji na usambazaji holela wa chumvi isiyo na madini joto kwa kiwango cha kutosha sambamba na matumizi ya sheria ya chumvi
Asilimia 18.4 ya wanawake wamekonda na pindi wapatapo ujauzito wako katika hatari ya kujifungua watoto wenye uzito pungufu na waliodumaa tumboni. Aidha pamoja na jitihada za sekta ya afya kutoa vidonge vya kuongeza damu kwa wajawazito, tafiti zinaonesha ni asilimia 27.2 tu ndo wanaoelewa umuhimu wa kumeza dawa hiyo kama wanavyoshauriwa na wataalamu. Wataalam wabuni mbinu bora zaidi za kuwashawishi wajawazito watumie hizi dawa ambazo ni muhimu kwa kuokoa uhai wa mama na mtoto aliye tumboni.

***Ndugu washiriki***

Bado jamii zetu hazioni umuhimu wa kuwa na vyoo lakini pia hazitumii sabuni wakati wa kunawa mikono hasa baada ya kutoka chooni na kabla ya kula chakula, hali inayoweza inayopelekea magonjwa ya kuhara ambayo yana uhusiano wa moja kwa moja na tatizo la udumavu kwa watoto.

*Ndugu Washiriki*

Ikumbukwe kuwa; mnamo tarehe 19/12/2017, Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa niaba ya Makamu wa Rais alisaini Mkataba wa utekelezaji afua za lishe na Wakuu wa Mikoa yote nchini. Mkataba wenye lengo la kuchochea utekelewa shughuli za lishe kwa kasi hapa nchini utadumu kwa mda wa miaka minne (01 Januari, 2018 hadi Juni 30, 2021; na una viashiria kumi (10) ambavyo wakuu wa Mikoa wanapimwa kila baada ya miezi 6, majukumu Natoa rai kwa watendaji wa ngazi zote na haswa kamati za lishe kutenga fedha kwenye mipango na bajeti kufuatana na miongozo yaani Tsh. 1000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano. Fedha hizi zitengwe kutoka kwenye vyanzo vinavyooaminika na usimamizi wa utekelezaji wa kila kiashiria uimarishwe zaidi. Ni matarajio yangu kuwa kila robo nipata taarifa ya utekelezaji na nataka nione matokeo yenye tija.

*Ndugu washiriki*

Bajeti za utekelezaji wa afua za lishe zilenge maeneo makuu matatu kama yalivyoainishwa katika mpango jumuishi wa lishe wa Taifa wa miaka mitano (NMNAP 2015/16-2020/21):

- ✓ Afua zenye matokeo ya haraka (Nutrition Specific interventions)
- ✓ Afua zinazochangia matokeo chanya (Nutrition sensitive interventions)
- ✓ Afua zinazoweka mazingira wezeshi katika utekelezaji (Enabling Environment interventions)

*Ndugu wahiriki*

Nitoe rai kwenu, kwamba fursa hii itumike vizuri; tushiriki kikamilifu mada zote na maelekezo yatakayotolewa na wawezeshaji wetu na baadaye tukaweke mipango inayotekelezeka ili itusaidie kuondokana na matatizo ya utapiamlo katika Wilaya wetu. Lakini pia niwatake watendaji na wataalamu wa Halmashauri yetu kuhakikisha mipango hii

mtakayoitengeneza inajumuishwa kwenye mipango ya Halmashauri ili na mimi niweze kufuatilia kwa karibu.
Nichukue fursa hii kuwatakia kila la heri na mafanikio katika kikao hiki. Twendeni tukiwa tunakumbuka kuwa lishe bora ni msingi wa maendeleo ya Wilaya yetu na Taifa kwa ujumla.

Baada ya kusema hayo;
***NAPENDA KUTAMKA KUWA KIKAO KAZI CHA HATUA ZA AWALI ZA UAANDAAJI NA UJUMUISHWAJI WA AFUA ZA LISHE KATIKA MIPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/20 KIMEFUNGULIWA RASMI.***

***ASANTENI KWA KUNISIKILIZA!***